

**MATUKIO KATIKA PICHA YA ZIARA YA KAMATI YA  
FEDHA NA UTAWALA MANISPAA YA SINGIDA  
TAREHE 09/05/2023**



Mwenyekiti wa kamati ya fedha , Utawala na Mipango, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Maulid Kiaratu pamoja na wajumbe wa kamati hiyo, wakioneshwa mipaka ya eneo la zahanati ya Unyamikumbi inayaotarajiwa kupandiswa hadhi na kuwa kituo cha afya



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida , Yagi Maulid Kiaratu akizungumza na wananchi wa kata ya Unyamikumbi waliofika katika zahanati ya Unyamikumbi kupata huduma za afya





Wajumbe wa kamati ya Fedha , Utawala na Mipango walipotembelea mradi wa jengo jipya la utawala la Manispaa ya Singida. Halmshauri ya Manispaa iya Singida imepokea fedha kiasi cha Tshs. Bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo kwa awamu ya kwanza





Jengo la maabara na OPD katika kituo kipya cha afya cha Kata ya Mtipa yanayojengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Manispaa yakiwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji ya uwekaji milango. Kiasi cha Tshs. 250,000,000/- kimetumika kwa ujenzi wa majengo hayo mawili pamoja na kichomea taka kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili inayohusisha jengo la mama na mtoto , upasuaji na jengo la kufulia tayari umeanza utekelezaji





Wajumbe wa kamati ya fedha wakitembelea Hospitali ya Manispaa ambayo awali ilikuwa hospitali ya Mkoa wa Singida.